CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA

TAARIFA KWA UMMA

Jumuiya ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) pamoja na Umma kwa ujumla mnataarifiwa kuwa kuanzia mnamo mwezi Januari 2018 malipo yoyote kwa ajili ya huduma mbalimbali zitolewazo na Chuo yamekuwa yakifanyika kwa njia ya Kielektroniki kupitia mfumo ulioanzishwa na Serikali ujulikanao kama Government e-Payment Gateway.

Kwa sababu hiyo, wanafunzi pamoja na wadau mbalimbali mnataarifiwa kwamba, kabla ya kufanya malipo kwa Chuo, mpate namba ya malipo (control number) kutoka kwenye mfumo wa taarifa za wanafunzi (Student Information System i.e SIS) kwa wanafunzi ama kutoka kwenye mfumo wa malipo (IFM Payment Portal) inayopatikana kupitia kwenye tovuti ya Chuo kwa wale wasio wanafunzi.

Namna ya Kupata Bili ya Malipo kwa Kutumia Mfumo wa Kielektroniki (Government e-Payment Gateway i.e GePG

Bili kwa Ajili ya Ada (Kwa Wanafunzi tu)

1. Ingia kwenye mfumo wa taarifa za mwanafunzi (www.ifmsis.ac.tz/studentis)
2. Fungua akaunti yako ya SIS
3. Bofya sehemu iliyoandikwa '**Fee Payments'** ili uweze kupata bili ya malipo.

Bili kwa ajili ya Malipo Mengine Yanayowahusu Wanafunzi

1. Ingia kwenye mfumo wa taarifa za mwanafunzi (www.ifmsis.ac.tz/studentis)
2. Fungua akaunti yako ya SIS

3. Bofya Sehemu iliyoandikwa '**Other Payments'**
4. Fuata maelekezo yanayotolewa kwa ajili ya kupata bili ya malipo.

Bili kwa Malipo Mengineyo kwa Wadau mbalimbali wasio Wanafunzi

1. Ingia kweye mfumo wa malipo kupitia www.ifmsis.ac.tz/payment_portal
2. Jaza fomu ya usajili wa malipo kwa usahihi
3. Bofya kitufe kilichoandikwa '**Submit**'
4. Subiria kwa dakika chache
5. Bofya kitufe kilichoandikwa **'here'** ili uweze kupata bili ya malipo

Maelezo ya Jinsi ya Kulipia Bili

Malipo yanaweza kufanyika kupitia banki au simu za kiganjani kwa kupitia mitandao mbalimbali.

Kwa njia ya simu za kiganjani au kuweka fedha Benki

Namna ya kulipia kwa Tigopesa

1. Piga *150*01#
2. Chagua namba (4) "Lipa Bill"
3. Chagua (5) "Malipo ya Serikali"
4. Ingiza namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number)
5. Ingiza kiasi cha pesa unachotaka kulipa
6. Ingiza namba ya siri kuhakiki

Namna ya kulipia kwa M-Pesa

1. Piga *150*00#
2. Chagua namba (4) "Lipa kwa M-Pesa"
3. Chagua (5) "Malipo ya Serikali"
4. Chagua namba 1 Namba ya Malipo
5. Ingiza namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number)
6. Ingiza kiasi cha pesa unachotaka kulipa
7. Ingiza namba ya siri
8. Thibitisha kwa kuchagua (1)

Namna ya kulipia kwa airtelmoney

1. Piga *150*60#
2. Chagua namba (5) “Lipia Bili”
3. Chagua (5) ”Malipo ya Serikali”
4. Chagua namba 1 “Weka namba ya kumbukumbu”
5. Ingiza namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number)
6. Ingiza kiasi cha pesa
7. Weka namba ya siri

Namna ya kulipia kwa T-Pesa

1. Piga *150*71#
2. Chagua namba (5) “Lipia Bili”
3. Chagua (3) ”Malipo ya Serikali”
4. Ingiza kumbukumbu namba (Control number)
5. Ingiza kiasi
6. Ingiza namba ya siri

Namna ya kulipia kwa halopesa

1. Piga *150*88#
2. Chagua namba (5) lipia bili
3. Chagua (5) malipo ya Serikali
4. Weka namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number)
5. Ingiza kiasi cha pesa
6. Weka namba ya siri

Namna ya kulipia kwa Ezypesa

1. Piga *150*02#
2. Chagua namba (8) malipo ya serikali
3. Chagua (1) Tanzania Bara
4. Weka namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number)
5. Ingiza kiasi cha pesa
6. Weka namba ya siri

Kwa njia ya Kuweka Fedha Benki (Direct Bank Deposit)

Malipo yanaweza kufanyika kwa njia ya kuweka fedha katika benki zifuatazo NMB /CRDB / TPB / NBC .Tumia namba ya kumbukumbu ya malipo (Control Number) uliyopewa ili kufanya malipo.

Kwa njia ya Kuhamisha Fedha(TISS/SWIFT)

Malipo yanaweza kufanyika kwa njia ya kuhamisha Fedha kutoka benki moja kwenda benki nyingine ndani ya Tanzania(TISS) au nje ya Tanzania(SWIFT),wakati wa kujaza fomu ya kuhamishia fedha lazima mambo yafuatayo yazingatiwe;

1. Taasis inayotoa huduma iandae bill(Transfer Bill) maalum kwa ajili ya wateja wanaolipia kwa njia ya kuhamisha fedha(TISS/SWIT) kwa kuzingatia fomu ya mfano("Kiambatanisho namba 2")
2. Kipengele cha 59(Field 59) kwenye fomu ya kuhamisha fedha(MT103) kijazwe akaunti ya mpokeaji(Beneficiary Account)
3. Kipengele cha 70(Field 70) kwenye fomu ya kuhamisha fedha (MT103) kijazwe namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number) na ijazwe kwa kutanguliza neon "ROC' yaani; /ROC/99XXXXXXXXX.
4. Mteja/Mlipaji apatiwe fomu za kuhamisha fedha baada ya kuichapa (Printed Transfer Form / Bill) aipeleke na kuiwasilisha katika benki atakayoitumia kuhamisha fedha na hatatakiwa kujaza upya fomu.

NB: Taasisi itatakiwa kuwasilisha orodha ya watumishi wake wanaohusika na masuala ya uhamishaji wa Fedha kuanzia wa ngazi ya chini mpaka wa ngazi ya juu katika utendaji kazi (Escallation Matrix) ili kurahisisha mawasiliano linapotokea tatizo lolote linalohusu uhamishashaji wa fedha.

Kwa Mawasiliano zaidi:

Mkuu wa Chuo
Chuo Cha Usimamizi wa Fedha
5 Shaaban Robert Street
S.L.P 3918
11101DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu: +255-22-2112931/3/4
Nukushi: +255-22-2112935
Barua Pepe: rector@ifm.ac.tz.
Tovuti: http://www.ifm.ac.tz